# NI MUHIMU MNO KILA MTEULE KUFANYA TATHMINI YA MAISHA YAKE YA KIROHO NA YA KIMWILI KILA MWAKA

## Maandiko: Mh. 7: 14 na Yosh 7: 6 – 13

1. **UTANGULIZI**

   Moja wapo ya siri ya ajabu iliyompa Yoshua mafanikio makubwa ya kiroho na kijeshi ni pale alipojenga tabia ya kukaa mbele za Mungu na kutathmini kwa nini Israeli wamepigwa na adui zao, na tena wanapigwa na adui ambao ni wachache mno!! Na Mungu akamjulisha sababu ya kupigwa kwao na kumwambia jambo la kufanya ili wasipigwe tena. ***Yosh 7: 14 – 26.***

- **Ni hatari sana kwa wana wa Mungu kama tutajiendea tu ili mradi miaka inapita; bali ni muhimu sana tena sana kuwa na muda wa kukaa chini na kutafakari juu ya maisha yetu ya wokovu kwamba ninapiga hatua za kuendelea mbele au nimesimama au tayari nimerudi nyuma katika mambo ya Mungu na huduma aliyonipa miaka ya nyuma. *1Kor 9: 26 – 27.***
- Eneo la kukaa chini na kufikiri (kujitathmini) kama mfalme Suleiman anavyotoa wito katika ***Mhubiri 7: 14*** ni eneo lililo na maana kubwa sana kama tunataka kufika kwa Baba; na bila kukaa chini daima na kujitathmini, wakati mwingine huwezi kujua kuwa umeshakosea mbele za Mungu na hivyo kukupelekea kukosa toba yako binafsi na kuendelea kuteseka bure. Nchi inayopiga hatua ni ile iliyo na tabia ya kufanya tathimini; hata waandaaji wa sherehe nyingi wana tabia ya kufanya tathmini kila baada ya sherehe zinapomalizika

2. Napenda mara nyingi kujifunza juu ya baraka ya huyu mwana mpotevu ambaye baba yake alimpokea na kumfanyia karamu na kumvika pete ya dhahabu baada ya kutapanya mali na kuishi maisha ya uasherati. ***Luk 15: 11 – 24 * 17 – 18.***

   Mwana mpotevu alipokaa chini na kutafakari maisha anayoishi akilinganisha na hali ya nyumbani aliyoiacha ndipo alipofanya maamuzi ya kurudi kwa Baba yake ili afadhali akawe mtumwa kwa Baba yake kuliko kuwa mtumwa wa dhambi. Hii ndiyo ikawa siri ya kubarikiwa kwake na kufanikiwa kwake.

- Ona anavyojiona baada ya kukaa chini na kujitathmini yeye mwenyewe kwanza kabla ya kuondoka na kumwendea Baba yake – ***Luk 15: 17 – 18*** **(And when he came to himself he said; How many hired servant of my fathers have bread enough and to spare; and I perish with hunger!! I will arise and go to my father and will say unto him "Father I have sinned against heaven and before thee; And am no more worthy to be called thy son; make me as one of thy hired servants.**

- **Na hii ndiyo hatua ya hali ya juu sana ya mtu wa Mungu aliye okoka pale anapoweza kukaa chini yeye mwenyewe na kuyatathmini maisha yake na kugundua mapungufu yake na kisha kuchukua hatua yeye peke yake na kumwendea baba wa kiroho na kutubu dhambi hiyo wazi pasipo kuhitaji aheshimiwe au afichiwe, bali awe radhi kwa hatua zozote atakazochukua Baba yake!! Ni hatua ya ufahamu wa hali ya juu sana tena sana kiroho mbele za Mungu. Na ni wachache sana katika Biblia waliofikia kiwango hiki cha ufahamu wa kiroho namna hii.**

3. Naipenda sana tabia ya ajabu ya kutathmini maisha yake aliyokuwa nayo mfalme **Daudi** hata baada ya kufanikiwa sana **kiroho, kivita, kifedha na kimaisha** kwa ujumla ***2Saml 7 :1 – 3 (5: 11 – 12)*** kama kuna siri iliyomfanya mfalme Daudi asiwe na kiburi hata alipokuwa amefanikiwa sana; ni siri ya kutathmini Bwana alikomtoa na sasa yuko wapi!! Hali hii ndiyo iliyomfanya Mungu ambariki daima mfalme Daudi tofauti na wafalme wengine wote wa kabla yake na baada yake. ***2Samwel 7: 14 – 16.***

- Hali ya kukaa chini na kutathmini maisha yake wapi Mungu alimtoa na akina nani waliokuwa na mchango mkubwa katika mafanikio ya maisha yake ndiyo iliyomfanya siku moja atende jambo hili la kihistoria ambalo halikuwahi kutendwa na mfalme mwingine yeyote katika Israeli – ***2Samwel 9: 1 – 14.***

- Mfalme Daudi alipokaa chini na kutafakari mchango wa rafiki yake Yonathani ambaye aliyatoa maisha yake kwa ajili yake na kuwa radhi kukosana na Baba yake mzazi Sauli kwa sababu ya upendo wake kwa Daudi, na kuwa tayari kumficha ili Baba yake asimuuwe, na kuwa tayari kupoteza nafasi yake ya kuwa mfalme baada ya Baba yake kufa ili Daudi apate. Daudi akasema nitakula na mtoto wa Yonathani meza moja hata kama ni mlemavu ili kila ninapomwona; nikumbuke mchango wa Baba yake Yonathani katika mafanikio yangu. ***1Samwel 18: 3 – 4, 20: 1 – 42.***

- Hata toba ya Daudi ilikuwa ya pekee sana pale alipoambiwa kwamba amemtenda Mungu dhambi mbaya na ya aibu. Daudi aliungama kwa kulia sana na kwa machozi ya siku nyingi. ***2Samwl 12: 1 – 15, Zab 51: 1 – 12;*** Na moja ya kilio chake kikubwa anamwomba Mungu asimtenge na uso wake, na wala asimwondolee Roho Mtakatifu. ***Zab 51: 11.*** Mfalme Daudi alifahamu fika kwamba tangu siku Samweli alipompaka mafuta kati ya ndugu zake, Roho Mtakatifu alimjilia kwa nguvu na kumfanya awe wa tofauti kabisa hali iliyomwezesha kupambana na **simba na dubu na Goliathi na kuwashinda; hali iliyomwezesha kumwabudu Mungu na kuimba Zaburi nyingi; akajua endapo Mungu atamwondolea Roho Mtakatifu atabaki debe tupu!!** Je mimi na wewe tunapata nafasi ya kutathmini maisha yetu kabla ya Yesu kutuokoa tulikuwaje na baada ya kutuokoa tukoje; Je ni nini sababu ya kuwa hivi tulivyo? Au tunazoea tu wema na fadhili za Mungu wetu!!

**Note: Ni hatari sana kufurahia pambio na nyimbo na mahubiri pasipo kutathmini maisha yetu kama kweli bado tunao ushirika mzuri na Roho Mtakatifu katika maisha yetu au tayari alishatuacha.**

- Kama hatuna muda wa kukaa chini na kutathmini **ndoa zetu; upendo wetu kwa Yesu na Neno lake; upendo wetu wa maombi pamoja na maombi ya kufunga; utoaji wetu mbele za Mungu atuonae jinsi tunavyomtolea ukilinganisha na jinsi alivyotubariki; mzigo wetu kwa ndugu zetu ambao wanateswa na dhambi; kwa nini ugonjwa huu unaniandama mara kwa mara; kwa nini natibiwa lakini siponi; kwa nini Napata kazi na baada ya muda mfupi tu nafukuzwa; au kwa nini naanza biashara na mtaji unapotea kiajabuajabu; hata kujitathmini tu kwa nini wapendwa hawaji nyumbani kwangu nk.** Ukijenga tabia ya kukaa chini na kujitathmini mwenyewe mbele za Mungu kama alivyofanya Yoshua, kwa vyovyote Mungu atakuonyesha sababu ya mambo hayo kukupata, mengine kwa ajili ya utukufu wake na mengine ni kwa sababu ya makosa yetu. ***2Kor 12: 7 – 10***

4. Leo hii wapendwa tunaingia **gharama** kubwa na kwa fedha nyingi kutibiwa **pressure, diabetes (sukari), vidonda vya tumbo, pumu, typhoid ndiyo usiseme, UTI, pneumonia, malaria, safura n.k** lakini kuingia gharama ya kwenda kwa ndugu yako tu ambaye umemkosea/ amekukosea tena bila fedha na kumsamehe/ na kutubu kosa lako mbele yake tumeshindwa!! Tunakaa na maadui mioyoni na bado tunaimba na kutoa sadaka tukidhani Roho Mtakatifu bado tunaye!! Daudi alijua tangu alipotenda dhambi Roho Mtakatifu aliondoka. Bila kujitathmini tutabakiza mazoea ya kuabudu; mazoea ambayo yalimfanya Samson ateseke baadae hadi kufa kabla ya kumaliza huduma aliyokuwa amepewa. ***Waamu 16: 20***

- Ni maombi yangu kwa Mungu anisaidie mimi pamoja na anayesikia ujumbe huu kuanzia leo **TUYATATHMINI** maisha yetu ya kiroho na ya kimwili kwa kukaa mbele za Mungu atujuae mapungufu yetu ili atujulishe sababu kwa nini mambo haya mabaya yanatupata mara kwa mara, au atujulishe vikwazo vilivyo mbele yetu au baraka inayotungoja na namna ya kuifikia. Amina.

***Na***
***Askofu Dr. L. Mwizarubi***
***20/01/2021***